



MISS TANZANIA

LINO INTERNATIONAL AGENCY LIMITED

P.O. BOX. 53069 DAR ES SALAAM, TELEFAX :+255 22 2120201,
SAMORA AVENUE AND MKWEPU, MOBILE: +255 753 764156, DAR ES SALAAM.

Email: linotz2000@yahoo.co.uk misstanzania@email.com

www.misstanzania.net

18 August 2010

Washiriki 30 wa Fainali za Vodacom Miss Tanzania 2010 tayari wameshaingia kambini katika hotel ya Kitalii ya Giraffe iliyopo eneo la Jangwani karibu na White sands.

Washiriki hao kutoka Kanda 9 na mikoa mbalimbali ya Tanzania watakuwa kambini kwa muda wa wiki 4 kuanzia Tarehe 16 Agosti hadi 11 Septemba 2010 siku ambayo Fainali hizo zitafanyika katika ukumbi wa Mlimani City uliopo jijini D'salaam.

Wakiwa kambini washiriki wote watapata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali yanayohusu masuala ya urembo ambayo yatakuwa yakitolewa na Wataalamu mbalimbali waliobobea katika masuala ya urembo.

Washiriki pia watapata fursa ya kutembelea vivutio vya Utalii vilivyopo hapa nchini kwa kutembelea mbuga za wanyama ya Manyara, Ngorongoro, na Hifadhi ya Arusha. Washiriki pia watatembelea eneo la Marangu gate sehemu ambayo Watalii mbalimbali huanzia safari ya kupanda Mlima wa Kilimanjaro.

Kama hiyo haitoshi, washiriki pia watapata nafasi ya kutembelea Mapango ya Amboni, [Amboni Caves] yaliyopo mkoani Tanga, na kujionea shughuli mbalimbali zinazofanyika huko.

Ziara hiyo itakayochukua takribani wiki 2 itajumuisha msafara wa watu 50 wakiwemo Warembo 30 Maafisa wa Kamati ya Miss Tanzania pamoja na Waandishi wa Habari za Magazeti na Televisheni.

Ratiba kamili ni kama ifuatavyo:

Tarehe	Shughuli	Mahali
20 Agosti	Washiriki Kuondoka DSM kuelekea Moshi Kilimanjaro Club La Liga –Redds Nite	Moshi – Snowview Hotel
21 agosti 2010	Washiriki Kutembelea eneo la Marangu gate kuona shughuli zinazofanyika	Moshi kilimanjaro

	hapo.	
22 agosti 2010	Washiriki Kuondoka Moshi kuelekea Arusha hadi Manyara	Manyara Njake Lodge
23 agosti 2010	Washiriki Kuondoka kuelekea Hifadhi ya Ngorongoro	Ngorongoro Crator
24 agosti 2010	Washiriki kutembelea Hifadhi ya Ziwa Manyara	Lake Manyara National Park
25 agosti 2010	Washiriki kutembela shule ya Mzee Laiboni kutoa misaada na kufanya kazi za jamii.	Makunyuni
26 agosti 2010	Waahiriki kutembelea Ofisi za Vodacom Arusha na Kituo cha Watoto Yatima cha Tumaini Gala Dinner	Arusha
27 agosti 2010	Washiriki kutembela mbuga ya Wanyama ya Arusha. Redds Nites	Arusha National Park Masai camp
28 agosti 2010.	Washiriki kuondoka Arusha kuelekea Tanga Amboni Caves Gala Dinner	Tanga Tanga Beach Resort
29 agosti 2010	Washiriki kurejea DSM Family day	Giraffe Hotel – Dsm

**Prepared by:
HIDAN .O. RICCO.
PRO.**